

KAULI YA WADAU KUHUSU MAENDELEO YA SEKTA YA MIFUGO TANZANIA

Wito wa kuchukua Hatua

Katika kauli hii, wadau waliotia sahihi (asasi za kiraia, wafugaji, watafiti, watu binafsi, vyama vya wakulima na wadau wengine) wanatoa wito wa kuchukua hatua pamoja na mapendekezo yao yaliyoainishwa katika mkakati wa uchechemuzi wa kiseru unaojali upekee na fursa katika maendeleo ya sekta ya mifugo nchini Tanzania.

Muhatasari

Sekta ya mifugo ni mhimili wa ukuaji wa uchumi nchini Tanzania ambako 50% ya kaya hutegemea aina fulani ya mifugo kama chanzo cha sehemu au kipato chao chote. Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan ambako bidhaa mbalimbali za mifugo kama vile nyama, kuku, nguruwe, mayai na bidhaa za ngozi huzalishwa lakini bado nchi hii inategemea uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ili kukidhi ukuaji wa mahitaji yake. Leo hii, sekta ya mifugo inahitaji kupewa msukumo ili kutoa fursa kwa nchi kufanikiwa kupitia uwezo wake kama kichocho cha ukuaji wa maendeleo jumuisi.

Sekta ya mifugo inaonekana kuchangia kufikia Dira ya Maendeleo Tanzania ya mwaka 2025 na uchambuzi uliofanjwa hivi karibuni umeonesha kuwa sekta hii huchangia kati ya asilimia 7.4 hadi asilimia 10 ya pato la taifa lakini bajeti ya maendeleo kwa sekta hii imebakia kuwa ndogo na kuendelea kushuka hadi kufikia TZS 10.6 bilioni kwa mwaka wa fedha 2016/17. Sekta ya mifugo inakuwa na kubadilika kwa haraka sana wakati huo huo mahitaji ya chakula na mailighafi yatakanayo na mifugo ikiongezeka mara dufu kunakochangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watu wa kipato cha kati pamoja na ukwaji wa miji. Uwezo na mchango wa sekta ya mifugo katika kufika malengo ya maendeleo ni kiashiria cha fursa ya kipekee katika kuleta mabadiliko makubwa.

Usuli

Uzalishaji wa mifugo nchini Tanzania, kama ilivyo uzalishaji wa mazaao hufanywa zaidi na wakulima wadogo na wafugaji wa asili, wengi wao wakiwa wanawake, wanaokumbana na changamoto za upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani na

asili katika sekta ya mifugo kuinua mchango wao katika kuinua uchumi wa Tanzania.

1. **Kuutambua kwa mapana mchango mkubwa wa mifugo kwa uchumi wa taifa na hivyo kutafiriwa katika ongezeko la uwekezaji wa serikali na sekta binafsi kuisaidia sekta hii:**
Kuwekeza kwa wazalishaji wadogo inaweza kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya mifugo na kuwa chachu ya ukuaji wa uchumi, uhakika wa chakula na lische nchini, kukidhi mahitaji ya vyakula vya asili ya mifugo yanayoongezeka na kupunguza umaskini. Mwonekano wa kimkakati wenye kujali mchango wa sekta ya mifugo katika uchumi wa Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima uwe kivutio cha kuongezeka kwa uwekezaji wa rasilimali za serikali na za sekta binafsi pamoja na utengenezaji wa sera na mikakati za kuwezesha kuwaunganisha wote pamoja.
2. **Kuongeza ushiriki wa wadau wasio wa serikali katika kutambua na kuunda sera za mifugo rafiki kwa wakulima wadogo na wafugaji wa asili chini:**
Inafahamika dhahiri kuwa uboreshaji wa mifugo, huduma za afya na mikakati ya malisho pamoja na upatikanaji wa huduma za ugani na masoko husaidia kuwezesha wakulima wadogo na wafugaji wa asili kuongeza uzalishaji kukidhi ongezeko la mahitaji ya bidhaa za mifugo.
Vivyo hivyo, kupunguzwa kwa gharama sizizo za lazima katika mnyororo wa thamani ina manufaa kwa wakulima wadogo na wafugaji wa asili katika kuwasaidia kukidhi ongezeko la mahitaji kupitia uzalishaji wa ndani. Kupitia mjadala mpana na ushirikiano kati ya asasi za kiraia, serikali, sekta binafsi na wadau wengine huwezesha zaidi taarifa za kuimarisha uthibiti wa kimazingira kwa wakulima wadogo na wafugaji wa asili kujumuishwa katika kukuza mnyororo wa thamani na viwanda na muunganiko imara.

3. **Ushiriki wa Wanawake na Vijana katika Mnyororo wa thamani wa mifugo:**

Wakati wanawake ni wadau wakuu katika uzalishaji wa mazwiwa na kuku, sera za mifugo hazielezi dhahiri ni kwa iinsi gani wanawake wanawezeshwa kushiriki

